# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 996

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-795-1

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VI Tanzania Bara.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

## ELIMU YA MSINGI

## DARASA LA III-VI

## 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-795-1

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejerelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VI.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali ........ iv
Vifupisho ........ v
Shukurani ........ vi
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla Elimu ya Msingi Darasa la III-VI ........ 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 4
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5
6.1 Mwalimu ........ 5
6.2 Mwanafunzi ........ 6
6.3 Mzazi/Mlezi ........ 6
7.0 Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7
8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7
9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8
10 Idadi ya Vipindi ........ 8
11 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Umahiri Husika ........ 9
Bibliografia ........ 43

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 4
Jedwali Na. 2: Maudhui kwa Darasa la III ........ 10
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa IV ........ 21
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Darasa la V ........ 28
Jedwali Na. 5: Maudhui ya Darasa la VI ........ 34

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| **LAT** | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la III-VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wakuza mitaala wa TET, wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wataalamu kutoka asasi za kiraia. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Historia ya Tanzania na Maadili ni la lazima katika ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI. Somo hili litafundishwa kwa Kiswahili ili kujenga na kuendeleza mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania. Lengo la kufundisha somo hili ni kumjenga Mtanzania kuwa mzalendo na muwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya Tanzania. Pia, linalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga maadili, kukuza Utaifa na uzalendo pamoja na kulinda rasilimali za nchi na za Taifa. Hivyo, kumwezesha mwanafunzi kuishi kwa kufuata misingi ya kuthamini kazi, uwajibikaji, utu, uadilifu, umoja, uzalendo, upendo na kuthamini rasilimali za Taifa.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi Darasa la I–VI, Tanzania Bara. Aidha, muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023 ambao msingi wake mkuu umejikita kupata wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku katika mazingira yake.

## 2.0 Malengo ya Elimu Tanzania

Malengo ya Elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, maendeleo endelevu ya Taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) Kufahamu, kutumia na kuthamini lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;

(c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kukuza maadili, uadilifu, na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

(g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na katika maisha ya kila siku;

(i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 4.0 Umahiri wa Jumla Elimu ya Msingi Darasa la III-VI

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Darasa la III-VI ni:

(a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) Kutumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza, na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;

(g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi kwa Darasa la III-VI una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyooneshwa katika jedwali namba 1.

**Jedwali Na 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kumudu dhana ya historia ya Tanzania urithi na maadili<br>1.2 Kumudu maarifa ya jamii inayomzunguka<br>1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa jamii inayomzunguka kusimulia asili, urithi na maadili ya jamii husika<br>1.4 Kutathmini ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi |
| 2.0 Kumudu historia ya Tanzania na Maadili kabla ya ukoloni | 2.1 Kuelezea mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>2.2 Kueleza maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni. |
| 3.0 Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni 1890-1960 | 3.1 Kuelezea historia ya Tanzania na urithi wakati wa ukoloni<br>3.2 Kulinganisha mabadiliko na mwendelezo wa maadili kabla na wakati wa ukoloni<br>3.3 Kuelezea jitihada za kulinda maadili ya Kitanzania dhidi ya maadili ya kigeni yaliyoletwa wakati wa ukoloni |
| 4.0 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili katika kipindi cha 1961-1966 | 4.1 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili mara baada ya uhuru katika kipindi cha 1961-1966<br>4.2 Kuelezea mchango wa Tunu na Alama za Taifa katika kujenga umoja wa kitaifa na uzalendo<br>4.3 Kutumia Alama za Taifa kama utambulisho wa Tanzania |
| 5.0 Kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili wakati wa Azimio la Arusha 1967-1985 | 5.1 Kuelezea misingi na maadili ya Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea<br>5.2 Kuelezea mchango wa Tanzania katika mapambano dhidi ya ukoloni na ukandamizaji |
| 6.0 Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali 1986 hadi sasa | 6.1 Kufafanua dhana ya ulibelali kwa kuhusianisha na maadili ya Kitanzania<br>6.2 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia ya Tanzania na maadili kufanya uamuzi sahihi katika nyakati za uliberali |
| 7.0 Kumudu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 7.1 Kufafanua dhana ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<br>7.2 Kuelezea utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jamii |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo.

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

(i) Kujenga umahiri unohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) Kushiriki ipasavyo katika tendo zima la ujifunzaji.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni.;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa;

(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji; na

(d) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

### 6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi/ Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto juu ya umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi ulenge kutumia mbinu zitakazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atumie mbinu zitakazomshirikisha mwanafunzi katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi. Pia, mbinu hizo zimwezeshe mwanafunzi kufikiri, kutafsiri, kutafuta maarifa, kujadili na kutumia maudhui ya somo Historia ya Tanzania na Maadili. Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji yanasisitizwa kuwezesha wanafunzi kupata na kutumia taarifa mbalimbali katika ujifunzaji wao.

Baadhi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa kutumika ni ziara za kimasomo, midahalo/klabu za masomo, tafiti ndogo, majadiliano, kisamafunzo, igizodhima, kazi za vitendo na kazi nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji. Pia, mwalimu atumie vyanzo na nyaraka za kihistoria kuwezesha ufundishaji na ufundishaji wa somo hili. Aidha mnwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji, umri, na uwezo wa mwanafunzi. Mwalimu anapaswa kuhakikisha mwanafunzi anapata nafasi ya ama kuona, kuhisi, kusikia na kushika zana wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwanafunzi kuelewa kile kinachofundishwa. Aidha, mwalimu anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka, pamoja na vitabu vya kiada,

ziada na vifaa vingine vya ufundishaji na ujifunzaji vilivyopata ithibati ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Baadhi ya zana zitakazotumika kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji ni muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza mwanafunzi katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na upimaji wa kitaifa wa Darasa la Sita ambao utachangia alama 7.5 katika mtihani wa Kidato cha Nne.

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi vitano (5) kwa wiki kwa Darasa la Tatu hadi la Sita.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Umahiri Husika

Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, vifaa/zana za ufundishaji na ujifunzaji vinazopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi kama Jedwali na. 2, 3, 4 na 5 linavyoonesha.

## Darasa la III

**Jedwali Na 2:** *Maudhui kwa Darasa la III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kulinda Historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kumudu dhana ya Historia ya Tanzania, urithi na maadili | (a) Kueleza dhana ya Historia ya Tanzania, urithi na maadili (maana, umuhimu) | **Bunguabongo:** Wanafunzi kubunguabongo maana ya historia ya Tanzania, urithi na maadili<br>**Changanyakete:** Wanafunzi katika vikundi wajadiliane kuhusu umuhimu wa historia ya Tanzania, urithi na maadili kisha washirikishe vikundi vingine ili kuboresha kazi zao<br>**Kutumia TEHAMA:** Wezeshe wanafunzi kujadili na kubaini dhana ya Historia ya Tanzania, urithi na maadili katika makala za filamu | Dhana ya Historia ya Tanzania, urithi na maadili imeelezwa | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Picha zinazoonesha historia ya Tanzania maadili na urithi<br>- Filamu zinazoonesha vitendo vya kimaadili | 10 |
| | | (b) Kubaini vitendo vya kimaadili na umuhimu wake | **Kisamafunzo:** Wanafunzi wajadili kisamafunzo chenye matukio ya kimaadili ili kujifunza vitendo vya maadili na umuhimu wake | Vitendo vya kimaadili na umuhimu wake vimebainishwa | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Igizodhima:** Ongoza wanafunzi kuonesha matendo ya maadili<br>**Kutumia TEHAMA:** Wezesha wanafunzi kujadili na kubaini vitendo vya kimaadili na umuhimu wake katika makala ya filamu | | - Michoro/picha/ picha mguso zinazoonesha vitendo vya kimaadili<br>- Filamu zinazoonesha vitendo vya kimaadili | |
| | 1.2 Kumudu maarifa ya jamii inayomzunguka | (a) Kubaini wajibu na haki zake katika familia na shuleni | **Utafiti mdogo:** Wanafunzi kuchunguza na kuandika kuhusu wajibu na haki zao katika familia na shuleni<br>**Changanyakete:** Wanafunzi katika vikundi wajadiliane kuhusu haki na wajibu wao katika familia na shuleni kisha washirikishe vikundi vingine kuboresha | Amebainisha wajibu na haki zake katika familia na shuleni | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Chati yenye kuonesha wajibu wa mtoto katika shule na familia | 50 |
| | | (b) Kuonesha matendo ya kuheshimu wengine, kutii sheria, | **Igizo dhima:** Wanafunzi waigize matendo ya heshima, kutii sheria, kujali na kushirikiana | Matendo ya kuheshimu wengine, kutii sheria, kujithamini, | - Matini yenye sheria za shule | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kujithamini, kujali na kushirikiana na watu wengine nyumbani na shuleni | **Maswali na Majibu:** Tumia maswali kuongoza wanafunzi kubaini matendo ya heshima, kutii sheria, kujali na kushirikiana<br>**Majadiliano:** Ongoza majadiliano kuwezeshwa wanafunzi kubaini matendo ya heshima, kutii sheria, kujali na kushirikiana | kujali na kushirikiana na watu wengine nyumbani na shuleni yameoneshwa | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Picha zenye kuonesha matendo ya kuheshimu, kuheshimiana na kushirikiana | |
| | | (c) Kueleza maarifa na ujuzi wa asili wa jamii inayomzunguka (katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa na dini) | **Utafiti mdogo:** Wanafunzi wachunguze na kuandika taarifa zinazohusu maarifa na ujuzi wa asili wa jamii katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa na dini<br>**Matembezi ya galari:** Wanafunzi wapitie kazi za vikundi vingine ili kujadili na kueleza | Maarifa na ujuzi wa asili wa jamii inayomzunguka katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa na dini yameelezwa | - Mazao mbalimbali<br>- Picha zenye kuonesha mazao ya kilimo, dawa na utunzaji wa mazingira | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | maarifa na ujuzi wa asili wa jamii katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa na dini | | - Filamu zenye kuonesha shughuli za kilimo, utunzaji wa mazingira<br>- Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | 1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa asili wa jamii inayomzunguka kusimulia asili, urithi, na maadili ya jamii husika | (a) Kubaini asili za jamii zinazomzunguka (tamaduni, mavazi, chakula, ngoma, michezo na nyimbo) | **Igizo dhima:** Ongoza wanafunzi kuigiza tamaduni za jamii zinazomzunguka.<br>**Utafiti mdogo**: Ongoza wanafunzi kuchunguza asili za jamii zao kupitia kwa walezi/wazazi na watu wengine<br>**Kutumia TEHAMA:** Wanafunzi wabainishe asili za jamii zinazowazunguka (mf. tamaduni, mavazi, chakula, ngoma, michezo | Asili za jamii (tamaduni, mavazi, chakula, ngoma, michezo na nyimbo) zinazomzunguka zimebainishwa | - Michoro/picha yenye ngoma za asili na michezo ya jamii<br>- Mavazi ya makabila ya Kitanzania<br>- Picha zenye kuonesha vyakula vya jamii tofauti<br>- Filamu zenye makala zinazohusu | 55 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na nyimbo za jamii katika makala za filamu walizozitazama | | asili za jamii | |
| | | (b) Kufafanua umuhimu wa maarifa, ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii | **Mtaalamu mwalikwa:** Alika mtaalamu kusimulia kuhusu umuhimu wa maarifa, ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria unavyosaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii<br>**Maswali na majibu:** Tumia maswali kuwezesha wanafunzi kufafanua umuhimu wa maarifa, ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii | Umuhimu wa maarifa, ujuzi wa asili na urithi wa kihistoria kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii umefafanuliwa | - Picha/ video zenye kuonesha urithi wa Historia na ujuzi wa asili<br>- Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | (c) Kubaini mbinu za kutumia maarifa na ujuzi wa asili (katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa, dini) | **Utafiti mdogo:** Wanafunzi kufanya uchunguzi ili kubaini mbinu za kutumia maarifa na ujuzi wa asili katika kuboresha ustawi wa jamii katika maeneo yanayowazunguka | Mbinu za kutumia maarifa na ujuzi wa asili (katika kilimo, utunzaji wa mazingira, dawa, dini) katika kuboresha | - Picha/picha mguso/ michoro yenye kuonesha shughuli za kilimo, | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | katika kuboresha ustawi wa jamii | **Changanyakete** : Wanafunzi katika vikundi wajadiliane kuhusu mbinu za kutumia maarifa na ujuzi katika kuboresha ustawi wa jamii kisha washirikishe vikundi vingine ili kuboresha | ustawi wa jamii zimebainishwa | utunzaji wa mazingira na dawa za asili<br>- Video zenye makala zinazohusu utunzaji wa mazingira | |
| | | (d) Kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira yake (mf. nyumbani, shuleni) | **Fikiri-Andika-Jozisha-Shirikisha** : Wanafunzi katika jozi wafikiri, waandike na kisha washirikishane namna ya kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira yao.<br><br>**Maswali na majibu** : Tumia maswali kuongoza wanafunzi kujadili namna ya kusimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira yao (mfano nyumbani na shuleni) | Anasimulia maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria katika mazingira ya shule na nyumbani | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Picha za vitu vya asili<br>- Filamu au michoro yenye maudhui yanayohusu maarifa na ujuzi wa asili, asili za jamii na urithi wa kihistoria | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kueleza thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayomzunguka | **Ziara za kimasomo**: Wanafunzi kutembelea maeneo yenye vitu vya asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayomzunguka na kuwasilisha taarifa<br>**Mgeni mwalikwa**: Alika mgeni kuelezea kuhusu thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayomzunguka<br>**Maswali na majibu** : Tumia maswali kuongoza wanafunzi kujadili na kueleza thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii inayomzunguka | Thamani ya asili na urithi wa kihistoria katika jamii imeelezwa | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Vitu vya asili na urithi wa kihistoria<br>- Picha/picha mguso zenye kuonesha maeneo ya urithi wa kihistoria | |
| | 1.4 Kutathmini ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | (a) Kueleza uhusiano wake na jamii inayomzunguka (nyumbani na shuleni) | **Uhalisishaji wa tukio:** Ongoza wanafunzi kwenye vikundi kuigiza uhusiano kati yao na baba, mama, dada, kaka, ndugu wa karibu na familia na watu wengine shuleni na nyumbani | Uhusiano wake na jamii inayomzunguka nyumbani na shuleni umeelezwa | - Picha/picha mguso/ michoro yenye kuonesha matendo ya kuhusiana | 30 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maswali na majibu:** Tumia maswali kuongoza wanafunzi kueleza uhusiano wao na familia, ndugu wa karibu na familia na watu wengine shuleni na nyumbani | | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | (b) Kubaini umuhimu wa uhusiano na ushirikiano wa familia na rafiki zake | **Kisamafunzo:** Wanafunzi wajadili visa mafunzo ili kubaini uhusiano na ushirikiano wa familia na rafiki<br>**Maswali na majibu** : Tumia maswali kuongoza wanafunzi kueleza umuhimu wa uhusiano na ushirikiano wa familia na rafiki zake | Umuhimu wa uhusiano na ushirikiano wa familia na rafiki zake umebainishwa | - Picha/picha mguso/ michoro yenye kuonesha matendo ya kuhusiana na ushirikiano<br>- Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | (c) Kueleza matendo ya kijamii na kiuchumi yanayojenga uhusiano na ushirikiano katika jamii | **Utafiti mdogo:** Wanafunzi kufanya utafiti mdogo maeneo ya sokoni, shuleni au kwenye shughuli za uzalishaji mali wakichunguza matendo ya kijamii na kiuchumi yanayojenga uhusiano na ushirikiano katika jamii | Matendo ya kijamii na kiuchumi yanayojenga uhusiano na ushirikiano katika jamii yameelezwa | - Picha/picha mguso/ michoro yenye kuonesha shughuli za kijamii na kiuchumi | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mtaalamu mwalikwa:** Alika mgeni kuelezea kuhusu matendo ya kijamii na kiuchumi yanayojenga uhusiano na ushirikiano katika jamii | | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| 2.0 Kumudu Historia ya Tanzania na Maadili kabla ya ukoloni | 2.1 Kuelezea mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kueleza mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia, ukoo na shule | **Igizo dhima:** Wanafunzi waandae na kuonesha igizo kuhusu mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia, ukoo na shule<br>**Utafiti mdogo:** Wanafunzi wachunguze na kuandika kuhusu mifumo ya uongozi katika ngazi za familia, ukoo na shule<br>**Kutumia TEHAMA:** Wanafunzi wajadili na kueleza mifumo ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania katika ngazi ya familia, ukoo na shule katika filamu walizozitazama | Mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia, ukoo na shule imeelezwa | - Chati yenye kuonesha mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia, ukoo na shule<br>- Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Makala zinazohusu mifumo ya utunzaji na ukuzaji wa maadili katika ngazi ya familia, ukoo na shule zilizoifadhiwa katika midia | 30 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili katika jamii inayomzunguka | **Changanyakete:** Wanafunzi katika vikundi wajadili misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili shuleni na nyumbani na kisha washirikishe vikundi vingine<br><br>**Mbinu za kutaja** *(snowball)*: Elekeza wanafunzi kila mmoja kueleza misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili shuleni na nyumbani<br><br>**Nyimbo:** Wanafunzi kuimba wimbo unaotaja misingi ya maadili shuleni na nyumbani | Misingi ya ukuzaji na utunzaji wa maadili katika jamii inayomzunguka shuleni na nyumbani imeelezwa | - Picha/picha mguso michoro yenye kuonesha misingi ya maadili<br>- Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Nyimbo za misingi ya maadili | |
| | | (c) Kueleza mchango wa uongozi wa ukoo katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii kabla ya ukoloni | **Utafiti mdogo:** Wanafunzi wachunguze na kuadika taarifa kuhusu michango ya viongozi wa koo zao katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii kabla ya ukoloni | Michango ya uongozi wa ukoo katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii kabla ya ukoloni umeelezwa | - Chati yenye kuonesha mifumo ya uongozi katika ngazi ya familia na ukoo | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mtaalamu mwalikwa:** Alika mgeni kuelezea kuhusu mchango wa viongozi wa ukoo katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii kabla ya ukoloni | | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili | |
| | | (d) Kubaini wajibu wa jamii katika ujenzi wa maadili ya familia | **Bunguabongo:** Ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu wajibu wa jamii katika ujenzi wa maadili ya familia<br>**Igizodhima:** Ongoza wanafunzi kuandaa na kuigiza matendo yanayohusu wajibu wa jamii katika ujenzi wa maadili ya familia<br>**Maswali na majibu:** Tumia maswali kuongoza washiriki kujadili kuhusu wajibu wa jamii katika ujenzi wa maadili ya familia | Wajibu wa jamiii katika ujenzi wa maadili ya familia umebainishwa | - Matini ya Historia ya Tanzania na Maadili<br>- Chati zenye kuonesha wajibu wa jamii katika ujenzi wa maadili | |

## Darasa la IV

**Jedwali Na 3***: Maudhui ya Darasa IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kulinda Historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kumudu maarifa ya jamii inayomzunguka | (a) Kutambua wajibu na haki zake katika jamii na Taifa | **Utafiti mdogo:** Ongoza wanafunzi kuchunguza na kuandika kuhusu haki na wajibu wao katika jamii na Taifa<br><br>**Kisamafunzo:** Ongoza wanafunzi kujadili kisamafunzo ili kutambua haki na wajibu wao katika jamii na Taifa.<br><br>**Majadiliano:** Tumia maswali kuwezesha wanafunzi kujadili na kutambua wajibu na haki zao wakati wa uwasilishaji<br><br>**Kutumia TEHAMA:** Wanafunzi wajadili ili kutambua wajibu na haki za mtoto katika jamii na Taifa katika filamu walizozitazama | Mwanafunzi ametambua wajibu na haki zake katika jamii na Taifa | - Chatipindu na manila zenye kuonesha haki na wajibu wa mtoto na wanafunzi<br>- Filamu zenye makala za haki na wajibu wa mtoto | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni | 2.1 Kuelezea mifumo mbalimbali ya utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kueleza mamlaka mbalimbali za kijadi kabla ya ukoloni (uchifu, usultani, utemi nk) | **Mtaalamu mwalikwa :** Alika mtaalamu kuelezea kuhusu mamlaka za jadi na kisha wezesha wanafunzi kujadili na kueleza kuhusu mamlaka za kijadi kama vile uchifu, usultani, utemi kabla ya ukoloni<br>**Oneshombinu :** Wanafunzi waandae na kuigiza nafasi za viongozi wa jadi na majukumu yao kabla ya ukoloni | Mamlaka mbalimbali za kijadi kabla ya ukoloni (uchifu, usultani, utemi nk) zimeelezwa | - Matini zenye kuonesha matukio ya kihistoria<br>- Picha na michoro inayohusu mamlaka za kijadi | 56 |
| | | (b) Kueleza michango ya mamlaka mbalimbali za kijadi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii kabla ya ukoloni | **Bunguabongo** : Ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu michango ya mamlaka za kijadi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili kabla ya ukoloni<br>**Majadiliano**: Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kueleza michango ya mamlaka za kijadi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii kabla ya ukoloni | Michango ya mamlaka mbalimbali za kijadi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii kabla ya ukoloni imeelezwa | - Chati zanye michoro yenye kuonesha mamlaka mbalimbali za kijadi<br>- Matini zenye taarifa za viongozi wa jadi na nafasi zao katika utunzaji na | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Matembezi ya galari** : Wanafunzi kuchambua katika vikundi michango ya viongozi wa jadi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii kabla ya ukoloni kwa kushirikisha vikundi vingine na kuboresha kazi zao | | ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii kabla ya ukoloni | |
| | | (c) Kufafanua wajibu wake katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii | **Utafiti mdogo** : Wanafunzi kuchunguza na kufafanua wajibu wao katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii<br>**Maswali na majibu** : Tumia maswali kuwezesha wanafunzi kujadili na kufafanua kuhusu wajibu wao katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii | Mwanafunzi amefafanua wajibu wake katika utunzaji na ukuzaji wa maadili ya jamii | - Matini au chati pindu zenye matendo ya wajibu wa mwanafunzi katika utunzaji na ukuzaji wa maadili | |
| | 2.2 Kueleza maendeleo ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni | (a) Kueleza dhana ya maendeleo ya jamii (maana, viashiria na umuhimu) | **Bunguabongo**: Ongoza wanafunzi kubunguabongo wakieleza dhana ya maendeleo ya jamii wakizingatia maana, viashiria na umuhimu | Dhana ya maendeleo ya jamii imeelezwa kwa kuzingatia maana, viashiria | - Matini zinazohusu maendeleo ya jamii | 99 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo-pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kutumia TEHAMA:** Waongoze washiriki kujadili na kueleza dhana ya maendeleo ya jamii kutokana na makala za filamu walizozitazama | vya maendeleo ya jamii na umuhimu | - Filamu zenye makala kuhusu maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | |
